



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE



*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. AC/18/214/ 74**

**Tarehe: 14/09/2022**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA USAFI KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NYANG'HWALE.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale anawatangazia Wananchi wa Wilaya ya Nyang'hwale nafasi za kazi.

Hivyo, anakaribisha maombi ya kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.

❖ **Wanaume wenye nguvu wafanya usafi- Nafasi tatu (3)**

**SIFA ZA MWOMBAJI**

- I. Awe na afya njema, mwaminifu, mwenye kujituyama.
- II. Awe ni Mwananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale (Mkazi)
- III. Awe na Kitambulisho cha NIDA

**MAJUKUMU YA KAZI**

- I. Usafirishaji/uondoaji taka ngumu
- II. Kuzoa taka katika eneo la Wilaya ya Nyang'hwale
- III. Kupeleka taka eneo la dampo
- IV. Kuhakikisha Trekta linakuwa safi na matunzo kwa ajili ya kazi

**MASHRTI YA JUMLA KWA MWOMBAJI**

- I. Mwombaji awe ni Mtanzania asiezidi umri wa miaka 45, awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale
- II. Mwombaji awe hajawahi kupatikana na kosa lolote la jinai, kufungwa jela au kupatikana na kosa lolote katika Utumishi wa Umma.
- III. Mwombaji anatakiwa aambatanishe cheti cha kuzaliwa na namba ya NIDA.

IV. Mwombaji ahakikishe ana Akaunti ya Benki iliyo hai (NMB au CRDB)

V. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 21/09/2022 saa 9:30 alasiri, Aidha maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo;-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 352

**NYANG'HWALE.**

Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri [www.nyanghwaledc.go.tz](http://www.nyanghwaledc.go.tz) na katika mbao za matangazo.



Mwizarubi Nyaindi

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
NYANG'HWALE.**

**MKURUGENZI MTENDAJI W**

**S.L.P 352**

**NYANG'HWALE.**